

فضل الشهادة ومنزلة الشهيد

وفلسفة الحرب في الإسلام

"Fadhila ya kufa shahidi na daraja ya Shahidi na Falsafa ya vita katika Uislamu"

Imefasiriwa na

Profesa. AYMAN ALASAR

Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa walimwengu wote, anayesema katika Qur'ani Tukufu:

"وَالشُّهَدَاءُ عِنْدَ رَبِّهِمْ لَهُمْ أَجْرٌ هُمْ وَنُورٌ هُمْ"

"**Mashahidi mbele ya Mola wao Mlezi. Wao watapata malipo yao na nuru yao**", na ninashuhudia kuwa hakuna Mungu ila Mwenyezi Mungu peke yake hana mshirika, na ninashuhudia kwamba Bwana wetu na Mtume wetu Muhammad ni mja na Mtume wake, Ewe Mwenyezi Mungu sala na salamu zimwendee yeye na familia yake na Maswahaba wake na kila atakayewafuata kwa wema mpaka siku ya malipo.

Amma bado

Ndugu zangu Waislamu, Kufa shahidi katika Njia ya Mwenyezi Mungu ni daraja ya juu kabisa, na lengo adhimu, ambapo Mwenyezi Mungu (S.W) humchagua amtakaye mionganini mwa waja Wake, kama katika kauli ya Mwenyezi Mungu (S.W) :

{وَيَتَخَذَ مِنْكُمْ شُهَدَاءَ}

، "Na awateuwe mionganini mwenu mashahidi", na ampabo anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

وَمَنْ يُطِعِ اللَّهَ وَالرَّسُولَ فَأُولَئِكَ مَعَ الَّذِينَ أَنْعَمَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ مِنَ النَّبِيِّينَ وَالصَّدِيقِينَ وَالشَّهِادَاءِ
وَالصَّالِحِينَ وَحْسُنَ أُولَئِكَ رَفِيقًا

"Na atakayemt'ii Mwenyezi Mungu na Mtume,basi hao watakuwa pamoja na wale Alio waneemesha Mwenyezi Mungu miongoni mwa Manabii, na Wasema kweli, na Mashahidi, na Watu wema. Na hao ndio wenye ukaribu na waja wema zaidi uzuri ulioje kuwa pamoja na watu hao!",

Na hakuna kinachoonesha ukubwa wa utukufu huu kuliko Shime ya Mtume S.A.W ya kutaka kufa Shahidi katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu ili amwandikie malipo ya kiwango cha juu, kwa hivyo amesema Mtume wetu (S.A.W): Ninaapa kwa Yule ambaye nafsi yangu iko mikononi mwake ningependelea niuawe vitani kwa ajili ya njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kisha niuishwe, kisha niuawe tena kisha niuishwe, kisha niuawe tena, kutokana na ukubwa wa malipo aliyoaandaa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa Mashahidi.

Hakika shahidi mkweli ni yule aliyekufa katika njia ya Mwenyezi Mungu, akitetea ardhi yake, heshima, pesa, au nchi yake, basi dhambi zake zitasamehewa na tone la kwanza la damu yake, ataona nafasi yake peponi, na atakuwa mwombezi kwa sabini kutoka familia yake, kwa hivyo, muamala ya mashahidi na Mola wao Mlezi ni hakika, ambapo Mwenyezi Mungu (S.W) anasema:

(إِنَّ اللَّهَ اشْتَرَى مِنَ الْمُؤْمِنِينَ أَنفُسَهُمْ وَأَمْوَالَهُمْ بِأَنَّ لَهُمُ الْجَنَّةَ يُقَاتِلُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَيُقْتَلُونَ وَيُقْتَلُونَ
وَعَدَ اللَّهُ عَلَيْهِ حَقًّا فِي التَّوْرَاةِ وَالْإِنْجِيلِ وَالْقُرْآنِ وَمَنْ أَوْفَى بِعَهْدِهِ مِنَ اللَّهِ فَاسْتَبْشِرُوا بِبِعْدِكُمُ الَّذِي يَأْتِيْكُمْ بِهِ
وَذَلِكَ هُوَ الْفُوزُ الْعَظِيمُ)

"Hakika Mwenyezi Mungu amenunua kwa Waumini nafsi zao na mali zao kwa kuwa wao watapata Pepo. Wanapigana katika Njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu , wanauwa na wanauwawa. Hii ni ahadi ya Mwenyezi Mungu ame

jilazimisha kwa Haki katika Taurati na Injili na Qur'ani. Na nani atimizae ahadi kuliko Mwenyezi Mungu? Basi furahini kwa biashara yenu mliyo fanya naye. Na huko ndiko kufuzu kukubwa", na anasema Mtume wetu (S.A.W):

(وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ لَا يُكَلِّمُ - أَيْ: يُجَرِحُ - أَحَدٌ فِي سَبِيلِ اللَّهِ - وَاللَّهُ أَعْلَمُ بِمَنْ يُكَلِّمُ فِي سَبِيلِهِ - إِلَّا

جَاءَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَاللَّوْنُ لَوْنُ الدَّمِ وَالرِّيحُ رِيحُ الْمِسْكِ)

"Napa kwa Mwenyezi Mungu kwamba mmoja wenu akijuruhiwa katika njia ya Mwenyezi Mungu – na Mwenyezi Mungu anamjua sana ni nani anayejuruhiwa katika njia yake- atakuja siku ya Malipo, rangi ni rangi ya damu lakini harufu ni harufu ya meski"

Ingawa Mashahidi wamefariki maisha yetu ya dunia, lakini wao ndio ni wahai kwenye Mola wao Mlezi (S.W), wanafurahi kwa zawadi zake, na wanafurahi kwa fadhila yake, ambapo Mwenyezi (S.W) anasema:

"Wala kabisa usiwadhanie walio uliwa katika Njia ya Mwenyezi Mungu kuwa ni maiti. Bali hao ni wahai, wanaruzukiwa kwa Mola wao Mlezi. * Wanafurahia aliyo wapa Mwenyezi Mungu kwa fadhila yake, na wanawashangilia wale ambao bado hawajajiunga nao, walio nyuma yao, ya kwamba haitakuwa khofu juu yao wala hawatahuzunika. * Wanashangilia neema na fadhila za Mwenyezi Mungu, na ya kwamba Mwenyezi Mungu hapotezi ujira wa Waumini.", na Mwenyezi Mungu (S.W) anasema pia:

"وَلَا تَقُولُوا لِمَنْ يُقْتَلُ فِي سَبِيلِ اللَّهِ أَمْوَاتٌ بَلْ أَحْيَاءٌ وَلَكِنْ لَا تَشْعُرُونَ"

{Na wala msiseme kwa wale wanaouawa katika njia ya Mwenyezi Mungu kuwa ni wafu bali wao wako hai lakini nyinyi hamuwezi kuhisi}.

Ndugu zangu Waislamu, kuna aina nyingi za Kufa shahidi, aina iliyo kubwa zaidi mionganoni mwa aina hizi ni kufa shahidi kwa ajili ya nchi, kuilinda ardhi yake, na kuwatetea watu wake, ili anaipata radhi ya Mwenyezi Mungu (S.W), ambapo Mtume wetu (S.A.W) anasema:

(مَنْ قُتِلَ دُونَ مَالِهِ فَهُوَ شَهِيدٌ، وَمَنْ قُتِلَ دُونَ دَمِهِ فَهُوَ شَهِيدٌ وَمَنْ قُتِلَ دُونَ دِينِهِ فَهُوَ شَهِيدٌ وَمَنْ قُتِلَ دُونَ أَهْلِهِ فَهُوَ شَهِيدٌ)

"Anayeuliwa kwa kuyatetea mali yake huyo ni Shahidi, aliyekufa kwa kutetea damu yake huyo ni Shahidi, anayeuliwa kwa kutetea Dini yake huyo ni Shahidi, na anayeuliwa kwa kumtetea watu wake huyo ni Shahidi",

Na mtu mmoja alimjia Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.A.W) akamwuliza: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, hebu niambie kama mtu atakuja anataka kuichukua mali yangu nimfanyeje?, akamjibu: usimpe mali yako, akauliza: je, akipigana name?, akamwambia: nawe pigana naye, akauliza: je, akiniuwa?, akamjibu: utakuwa Shahidi, akauliza: je, nikimwuua?akamjibu: ataingia motoni".

Ninasema kauli yangu hii na ninamwomba Mwenyezi Mungu Mtukufu anisamehe mimi na nyinyi

Ndugu zangu waislamu tunazungumza katika hotuba ya pili juu ya fadhila ya kufa shahidi kwa ujumla na daraja lake katika akhera na sababu ya kufaradhisha vita katika uislamu.

Sifa zote njema ni zake Mwenyezi Mungu Mtukufu Mola Mlezi wa viumbe vyote. **Na ninashuhudia ya kwamba hakuna mungu**

mwingine yoyote anaestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, yeye pekee asiye na mshirika wake. Na ninashuhudia ya kwamba Bwana wetu na Mtume wetu Muhammad ni Mja na Mjumbe wake. Ewe Mola Wetu Mlezi tunakuomba umswalie umrehemu na umbariki yeye na jamaa zake na Maswahaba wake wote na kila atakayewafuata mpaka siku ya Mwisho.

Ndugu zangu Waislamu:

Vita vimefaradhishwa katika Uislamu ili kuondoa dhulma na uchokozi, Uislamu hauna hamu ya kupigana au kumwaga damu, badala yake, huacha vita maadamu unaweza kufanya hivyo, ruhusa ya kupigana ni finyu na ina masharti, Mwenyezi Mungu (S.W) anasema:

{أَذْنَ اللَّهِ الَّذِينَ يُقَاتِلُونَ بِأَنَّهُمْ ظُلْمُوا وَإِنَّ اللَّهَ عَلَى نَصْرِهِمْ لَقَدِيرٌ}

Wameruhusiwa kupigana wale wanao pigwa vita kwa sababu wamedhulumiwa - na kwa yakini Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kuwasaidia", na anasema Mwenyezi Mungu (S.W):

{وَقَاتِلُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ الَّذِينَ يُقَاتِلُونَكُمْ وَلَا تَعْنَدُوا إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ الْمُعْتَدِلِينَ}

" Na piganeni katika Njia ya Mwenyezi Mungu na wale wanao kupigeni, wala msianze uadui. Kwani Mwenyezi Mungu hawapendi waanzao uadui.", Na anasema pia (S.W):

{وَإِنْ جَنَحُوا لِلسلِّمِ فَاجْنِحْ لَهَا وَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ إِنَّهُ هُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ}

"Na wakielekea amani nawe pia elekea, na mtegemee Mwenyezi Mungu. Hakika Yeye ndiye Mwenye kusikia Mwenye kujua.", na Mtume wetu (S.A.W) anasema:

(يَا أَيُّهَا النَّاسُ لَا تَتَمَنَّوْ لِقَاءَ الْعَدُوِّ، وَسَلُوا اللَّهَ الْعَافِيَةَ، فَإِذَا لَقِيْتُمُوهُمْ فَاصْبِرُوْا)

"Enyi watu msitamani kukutana na adui na muombeni Mwenyezi Mungu afya (kwa maana ya salama), na mtakapokutana nao msuburini,...".

Tunamwomba Mwenyezi Mungu Mtukufu awape Mashahidi wetu rehema pana zaidi na alinde na Shari Nchi yetu Pendwa na uwalinde watu wake, Majeshi yetu ya Usalama na ya Ulinzi wa Nchi, na wananchi wote na uidumishe neema ya amani na usalama na uiruzuku utajiri,maendeleo na riziki iliyo pana.Na mwisho wa dua yetu ni Alhamdulillahi Rabbi Alalameen.